

# TANGAZO LA KAZI



## WAKALA WA VIPIMO

Wakala wa Vipimo ni Taasisi (Wakala) ya Serikali iliyo chini ya Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji. Taasisi hii iliundwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala za Serikali Sura Na. 245, mapitio ya mwaka 2002. Wakala wa Vipimo ilianzishwa rasmi tarehe 13 Mei, 2002 kwa amri ya Serikali Na. 194 (Government Order No. 194) na kutangazwa tarehe 17 Mei, 2002. Wakala wa Vipimo ina jukumu la kumlinda mlaji kwa kuhakiki vipimo vyote vinavyotumika katika sekta za Biashara, Afya, Usalama na Mazingira.

Nafasi hizi zitajazwa katika ofisi za Wakala wa Vipimo zilizoko Makao Makuu na katika Mikoa yote Tanzania Bara.

### 1.0 AFISA VIPIMO DARAJA LA II:

Nafasi 10

#### (a) Sifa za kuingilia moja kwa moja

- Kuajiriwa wenye Stashahada ya Juu/Shahada ya kwanza ya *Legal and Industrial Metrology* toka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- Au kuajiriwa wenye Shahada ya Uhandisi/Sayansi waliohudhuria mafunzo ya Mwaka mmoja ya Stashahada ya Uzamili ya *Legal and Industrial Metrology* toka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

#### (b) Sifa za kuingilia waliomo kazini:

- Kubadilishwa vyeo Maafisa Vipimo Wasaidizi ambao watakuwa wamepata sifa zilizotajwa katika Kifungu 1 (a) hapo juu;
- Kubadilishwa vyeo watumishi toka kada nyingine watakao kuwa wamepata sifa zilizotajwa katika Kifungu 1(a) hapo juu.

(c) **Kazi za Kufanya:**

- (i) Kukagua, kuhakiki na kuvirekebisha vipimo vya wafanyabiashara;
- (ii) Kutunza na kuhifadhi vifaa vya kitaalam vitumikavyo katika utendaji wa kazi;
- (iii) Kutoa ushauri kuhusu masuala ya uhakiki na matumizi ya vipimo;
- (iv) Kufanya upelelezi kuhusu ukiukwaji wa Sheria ya vipimo;
- (v) Kupokea na kufanyia kazi malalamiko ya wadau na wateja.
- (vi) Kufanya kazi nyingine kama atakavyopangiwa na kiongozi wake zinazohusiana na elimu na ujuzi wake wa kazi.

**NGAZI YA MSHAHARA**

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Wakala wa Vipimo WMAS 3 kwa mwezi.

**MASHARTI YA KUOMBA KAZI**

1. Waombaji wote lazima wawe raia wa Tanzania wenye umri usiozidi miaka arobaini na tano (45).
2. Waombaji wanatakiwa kuambatisha nakala ya wasifu wa hivi karibuni yenye anuani ya sanduku la barua, barua pepe na namba za simu.
3. Waombaji wanatakiwa kuambatisha vyeti vifuatavyo ambavyo vimehakikiwa (certified copies):
  - Stashahada ya Uzamili (Postgraduate Diploma)
  - Cheti cha Stashahada ya Juu/Shahada ya kwanza
  - Cheti cha Elimu ya Ufundi
  - Cheti cha Kidato cha Nne na Cheti cha Kidato cha sita
  - Cheti cha kuzaliwa
4. Waombaji hawatakiwi kuambatisha nakala ya hati ya matokeo (result slips) ya kidato cha Nne na kidato cha sita au *Testimonials and all Partial transcripts*.
5. Waombaji ambao wameajiriwa katika utumishi wa Umma wapitishe maombi ya kazi kwa waajiri wao.
6. Wastaafu katika utumishi wa Umma kwa sababu zozote hawatakiwi kutuma maombi.
7. Waombaji wanatakiwa kuandika majina matatu ya wadhamini (referees).
8. Waombaji wenye mahitaji maalum/ulemavu wanashauriwa kuainisha.

9. Maombi ya barua yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili au kiingereza na yatumwe kwa:

Afisa Mtendaji Mkuu,  
Wakala wa Vipimo,  
S.L.P. 313,  
**DAR ES SALAAM.**

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 4 Septemba, 2017.

Waombaji watakaochaguliwa ndio tu watakaotaarifiwa kwa ajili ya tarehe ya usaili.

**AFISA MTENDAJI MKUU  
WAKALA WA VIPIMO**